/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 13*** ***19th October, 2023***

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 43 Vol. 104 Dated* ***19th October, 2023***
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

# MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI WA UMMA WA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
### MAMLAKA YA UWEKEZAJI WA UMMA

4. Uanzishwaji wa Mamlaka.
5. Majukumu ya Mamlaka.
6. Majukumu ya wizara ya kisekta.
7. Mamlaka ya Mamlaka.
8. Mamlaka kuhusu masuala ya kifedha katika mashirika.
9. Bodi ya Mamlaka.
10. Mamlaka na majukumu ya Bodi.
11. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.
12. Watumishi wa Mamlaka.
13. Uwekaji wa lakiri.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA MASHIRIKA YA UMMA

14. Shirika kushika mali kwa udhamini.
15. Kuhamisha mali za shirika la umma.
16. Uteuzi wa watendaji wakuu au wajumbe wa vyombo vya usimamizi.
17. Baadhi ya watu kukosa sifa.
18. Rejesta ya mashirika ya umma.
19. Mamlaka ya kuitisha taarifa.
20. Ukomo wa gharama za uendeshaji.

SEHEMU YA NNE
MFUKO WA UWEKEZAJI WA UMMA

21. Mfuko wa Uwekezaji wa Umma.
22. Madhumuni ya Mfuko.
23. Usimamizi wa Mfuko.
24. Utunzaji wa kumbukumbu na ukaguzi wa Mfuko.
25. Kamati ya Uongozi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma.
26. Majukumu ya Kamati ya Uongozi.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

27. Fedha za Mamlaka.
28. Hesabu na ukaguzi.
29. Taarifa ya mwaka.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

30. Makosa na adhabu.
31. Kanuni.
32. Kufutwa kwa Sheria na masharti ya muendelezo.
33. Masharti ya mpito.
34. Marekebisho ya jumla.

SEHEMU YA SABA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma, (Sura ya 257)*

35. Ufafanuzi.
36. Marekebisho ya kifungu cha 12.

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, (Sura ya 348)*

37. Ufafanuzi.
38. Marekebisho ya kifungu cha 6A.

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Kuunda Upya na Kuhamisha Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, (Sura ya 404)*

39. Ufafanuzi.
40. Marekebisho ya kifungu cha 3.
41. Kufutwa kwa Sehemu ya Pili.
42. Kufutwa kwa vifungu vya 12 na 13.
43. Kufutwa kwa Jedwali la Pili.

**TAARIFA**

Muswada huu unaokusudiwa kuwasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dodoma,
18 Oktoba, 2023

**MOSES M. KUSILUKA**
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

*Muswada*
*wa*

**Sheria ya kuweka masharti ya uwekezaji wa umma, mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji wa umma, usimamizi wa mashirika ya umma, kufuta Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, na masuala yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Uwekezaji wa Umma ya mwaka 2023 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika kwa mashirika ya umma yaliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria yoyote.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"chombo cha usimamizi" maana yake ni chombo kilichoteuliwa kusimamia uendeshaji wa shirika la umma;

"Kamati ya Uongozi" maana yake ni Kamati ya Uongozi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 25;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ulioanzishwa katika kifungu cha 21;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11;

"shirika la umma" maana yake ni shirika lolote la umma, wakala wa serikali au taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa sheria yoyote, ambapo Serikali au wakala wake unamiliki sehemu kubwa ya hisa au ni mmiliki pekee.

"uwekezaji wa umma" inajumuisha hisa, dhamana ya hisa, hisa ya dhamana, hisa za mkopo, hati ya malipo, hati fungani na rehani ya mali za shirika la umma au zilizotolewa na au kwa niaba ya Serikali;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji; na

"wizara ya kisekta" maana yake ni wizara yenye dhamana ya shirika la umma husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAMLAKA YA UWEKEZAJI WA UMMA

Uanzishwaji wa Mamlaka

**4**.-(1) Inaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma.

(2) Mamlaka itakuwa taasisi nafsi yenye muendelezo wa kurithi na lakiri na kwa jina lake itakuwa na uwezo wa-

(a) kumiliki au kuuza mali inayohamishika au isiyohamishika;
(b) kuingia katika mkataba au makubaliano yoyote;
(c) kushtaki na kushtakiwa; na
(d) kufanya jambo lingine lolote ambalo taasisi nafsi inaweza kufanya kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Majukumu ya Mamlaka

**5**.-(1) Mamlaka itafanya usimamizi wa jumla wa shughuli na masuala yote ya mashirika ya umma.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu uanzishaji au ufutaji wa mashirika ya umma na umilikishwaji wa biashara au mali yoyote katika mashirika ya umma;
(b) kufanya mapitio ya utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma kwa lengo la kubaini mahitaji na kupendekeza kwa Kamati ya Uongozi njia bora za uwezeshaji wa kifedha;
(c) kufanya mapitio na kuidhinisha mikakati, mipango ya mwaka na bajeti za mashirika ya umma au

taasisi nyingine ambazo Mamlaka ina maslahi na kuwasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya kujumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa;

(d) kuweka malengo ya kifedha na vigezo vingine vya utendaji vitakavyozingatiwa na mashirika ya umma;

(e) kuweka vigezo vya mashirika ya umma kupata fedha za uwekezaji kutoka katika Mfuko;

(f) kutathmini utendaji na ufanisi wa vyombo vya usimamizi vya mashirika ya umma na kupendekeza kwa Serikali hatua za kurekebisha au kuboresha kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha na mali za mashirika ya umma;

(g) kuidhinisha maombi ya shirika la umma ya kununua hisa;

(h) kuwekeza au kuondosha uwekezaji katika mashirika ya umma au maeneo mengine yenye fursa za kibiashara;

(i) kusimamia fedha za uwekezaji za mashirika ya umma;

(j) kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha michango ya mashirika ya umma na gawio kutoka katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa, vinalipwa kwa wakati;

(k) kufuatilia utendaji wa mashirika ya umma kwa madhumuni ya kutathmini uendelevu wake na kupendekeza hatua stahiki ikiwemo kuunganisha au kufuta mashirika husika au kuboresha utendaji;

(l) kuhakikisha kwamba kila shirika la umma linaingia mkataba wa utendaji kazi na Mamlaka;

(m) kuelekeza au kuidhinisha matumizi au marekebisho ya kanuni za fedha ili kuhakikisha utunzaji wa hesabu sahihi za mapato na matumizi ya mashirika ya umma;

(n) kwa kushauriana na Wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma, kutathmini na kuidhinisha muundo wa kitaasisi, mishahara, maendeleo ya utumishi, motisha na kanuni za utumishi katika mashirika ya umma na nyaraka nyingine kadri zitakavyohitajika;

(o) kusimamia misaada kwa ajili ya mtaji, ruzuku, fedha za mtaji na mapato ya mashirika ya umma na uwekezaji mwingine wowote wa umma;

(p) kupokea, kuhakiki na kuidhinisha maombi ya

Sura ya 134

mikopo kwa mashirika ya umma kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali;

(q) kubaini maeneo yenye tija kwa Serikali kuwekeza;

(r) kwa kushauriana na Wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma, kufanya mapitio na kuidhinisha maslahi ya wajumbe wa vyombo vya usimamizi wa mashirika ya umma;

(s) kuainisha mashirika ya umma ikiwa ni pamoja na kubainisha yale yanayojiendesha kibiashara na yasiyojiendesha kibiashara;

(t) kuamua namna ya kuendeleza mashirika ya umma yaliyofanyiwa maboresho au kuwekwa chini ya uangalizi;

(u) kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa;

(v) kusimamia utoaji wa hisa za Serikali kwa umma katika masoko ya hisa;

(w) kukusanya madeni ya mashirika ya umma yatokanayo na mikataba ya mauziano;

(x) kuwezesha upatikanaji wa hati miliki kwa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa;

(y) kukamilisha utekelezaji wa majukumu na kurithi mali na madeni ya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali; na

(z) kutoa miongozo na maelekezo ya usimamizi na uendeshaji wa mashirika ya umma.

Majukumu ya wizara ya kisekta

**6**. Bila kuathiri majukumu ya Mamlaka, wizara ya kisekta itakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya kisera yanayotekelezwa na shirika la umma.

Mamlaka ya Mamlaka

**7.** Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Mamlaka itakuwa na mamlaka ya-

(a) kufanya uwekezaji kwa niaba ya Serikali;

(b) kumuita mtendaji mkuu au mwenyekiti wa chombo cha usimamizi wa shirika la umma kwa ajili ya mahojiano kuhusu utendaji wa shirika la umma;

(c) kupendekeza kwa mamlaka ya uteuzi kutengua uteuzi wa mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe yeyote wa chombo cha usimamizi au kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi wa shirika la umma;

(d) kulitaka shirika la umma kutoa kumbukumbu au

taarifa yoyote kuhusu masuala ya shirika husika; na

(e) kufanya ukaguzi wa mashirika ya umma baada ya kutoa taarifa au bila kutoa taarifa.

Mamlaka kuhusu masuala ya fedha katika mashirika ya umma

**8**.-(1) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi bora wa mali na uwekezaji wowote unaosimamiwa na Mamlaka, Mamlaka itafuatilia usimamizi na udhibiti wa masuala ya fedha ya mashirika yote ya umma na inaweza-

(a) kuelekeza uchunguzi maalum kufanyika katika matumizi ya fedha za shirika lolote la umma;

(b) kulitaka shirika la umma kufanya marekebisho mahsusi katika matumizi ya fedha;

(c) kuelekeza au kuwezesha uchunguzi kufanyika kuhusu mwenendo na utekelezaji wa majukumu ya maafisa wanaosimamia fedha au walioajiriwa kutunza hesabu za shirika lolote la umma;

(d) kuelekeza au kuidhinisha matumizi au marekebisho ya kanuni za fedha ili kuhakikisha kunakuwa na usahihi wa hesabu za mapato na matumizi ya shirika la umma;

(e) kupendekeza kwa Waziri hatua kwa ajili ya-

(i) kupunguza matumizi ya mashirika ya umma yasiyo na tija; na

(ii) kuepusha upotevu wa fedha kutokana na uzembe, wizi, kukosa uaminifu au vinginevyo.

(2) Waziri anaweza, kupitia kanuni, kuweka utaratibu kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwepo na ufanisi katika utekelezaji wa mamlaka ya udhibiti na usimamizi yaliyotolewa chini ya kifungu hiki.

Bodi ya Mamlaka

**9**.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Mamlaka ambayo itakuwa na wajibu wa kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mamlaka.

(2) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka, ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) wajumbe wengine nane watakaoteuliwa na Waziri kama ifuatavyo:

(i) Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango;

(ii) Kamishna wa Sera anayesimamia masuala ya uchumi katika Wizara yenye dhamana ya fedha;

(iii) Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;

(iv) mwakilishi kutoka wizara yenye dhamana na utumishi wa umma; na

(v) wajumbe wengine wanne wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uwekezaji.

(3) Mkuu wa idara au kitengo cha sheria katika Mamlaka atakuwa ndiye Katibu wa Bodi.

(4) Ukomo wa muda wa kuhudumu, akidi, utaratibu wa vikao na masuala mengine ya Bodi yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Mamlaka na majukumu ya Bodi

**10**. Bodi itatekeleza mamlaka na majukumu yafuatayo:

(a) kutoa mwongozo wa kimkakati na kuandaa sera kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa Mamlaka;

(b) kuidhinisha mipango, taarifa, hesabu na bajeti ya Mamlaka;

(c) kutathmini utendaji wa uongozi na kuchukua hatua stahiki;

(d) kuteua wajumbe wa menejimenti ya Mamlaka;

(e) kuwa na mamlaka ya nidhamu kwa wajumbe wa menejimenti ya Mamlaka;

(f) kuidhinisha kanuni za maadili za watumishi wa Mamlaka;

(g) kuidhinisha na kusimamia kanuni za fedha;

(h) kutekeleza majukumu mengine yoyote kadri itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya Mamlaka.

Mkurugenzi Mtendaji

**11**.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Katika kumteua Mkurugenzi Mtendaji, Rais atazingatia sifa za kitaaluma, uzoefu na ujuzi wa uongozi unaohitajika kwa ajili ya uteuzi katika nafasi hiyo.

(3) Isipokuwa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 9(2)(a), Mkurugenzi Mtendaji hatateuliwa yeye binafsi au kwa nafasi yake kuwa mjumbe au Mwenyekiti wa chombo cha usimamizi wa shirika lolote la umma.

(4) Sharti la kifungu kidogo cha (3) litatafsiriwa kama ni zuio kwa afisa mwingine yeyote wa Mamlaka kuteuliwa kama mjumbe wa chombo cha usimamizi cha shirika la umma.

(5) Mkurugenzi Mtendaji atashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine kimoja.

Watumishi

**12**.-(1) Mamlaka itaajiri au kuteua maafisa au watumishi

wa Mamlaka

kwa idadi, kada na sifa kadri itakavyoonekana ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

(2) Katika kuajiri au kuteua maafisa na watumishi chini ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itaongozwa na sheria zinazosimamia ajira katika utumishi wa umma.

Sura ya 298

(3) Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, mtu ambaye, kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, anahudumu katika nafasi yoyote katika Ofisi ya Msajili wa Hazina, mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, atachukuliwa kuwa ameteuliwa au kuajiriwa na Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Uwekaji wa lakiri

**13.** Lakiri ya Mamlaka itakuwa imewekwa ipasavyo ikiwa imeshuhudiwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa niaba yake.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA MASHIRIKA YA UMMA

Shirika kushika mali kwa udhamini

Sura ya 257

**14.**-(1) Uwekezaji na mali nyingine zilizowekwa chini ya Mamlaka, ikijumuisha uwekezaji katika mtaji uliolipwa wa shirika la umma kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Mashirika ya Umma, vitamilikiwa kwa udhamini na Mamlaka kwa niaba ya Rais na kwa madhumuni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Rais anaweza, kwa maslahi ya umma na kwa mujibu wa Sheria husika, kutoa maelekezo kwa Mamlaka kuhusu uondoshaji wa uwekezaji au mali nyingine zinazomilikiwa na Mamlaka pamoja na riba, mapato au zao la uwekezaji au mali hizo.

(3) Isipokuwa kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (2), kifungu hiki au sheria nyingine yoyote inayohusu udhamini au wadhamini haitatafsiriwa kuwa-

(a) inamtaka Mkurugenzi Mtendaji kuondosha mali yoyote inayomilikiwa kwa udhamini kwa niaba ya Rais na kuwekeza mapato yake katika dhamana; au

(b) inamuwajibisha Mkurugenzi Mtendaji kwa kubaki na mali yoyote au kwa kutokuwekeza mapato ya mauzo ya mali au fedha yoyote inayomilikiwa kwa udhamini katika uwekezaji ulioidhinishwa kwa ajili ya wadhamini.

Kuhamisha mali za

**15.**-(1) Shirika la umma halitahamisha mali bila kibali cha Rais.

shirika la umma

(2) Endapo shirika la umma linakusudia kuhamisha mali, litawasilisha maombi kwa Rais kupitia Mamlaka.

(3) Maombi ya kuhamisha mali yataambatana na nyaraka zitakazoainishwa katika kanuni.

(4) Baada ya kupokea maombi chini ya kifungu kidogo cha (2), Mamlaka itafanya uchambuzi wa maombi hayo na endapo itajiridhisha na usahihi na tija ya uhamisho wa mali husika, itawasilisha kwa Rais kwa ajili ya kibali.

(5) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu hiki, baada ya Rais kutoa kibali cha kuhamisha mali, mali husika zitahamishwa kwa njia ya hati itakayosainiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa amri ya Rais na hati hiyo itatangazwa katika Gazeti la Serikali.

(6) Masharti ya kifungu hiki hayatatafsiriwa kuwa yanazuia utekelezaji wa majukumu ya mashirika ya umma ambayo msingi wa kuanzishwa kwake ni kununua na kuuza mali.

Uteuzi wa watendaji wakuu au wajumbe wa vyombo vya usimamizi

**16.-**(1) Endapo Serikali ni mmiliki pekee wa shirika la umma, Mamlaka itatumia taratibu za ushindani katika kupata majina ya watu wenye sifa za kuteuliwa kama mtendaji mkuu wa shirika la umma, wenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi na kuwasilisha majina hayo kwa wizara ya kisekta.

(2) Katika kupata majina ya watu wenye sifa za kuteuliwa, Mamlaka itajiridhisha kuwa kila mtu aliyependekezwa-

(a) ana ujuzi unaohitajika katika kusimamia shirika la umma husika;

(b) hashiki nafasi ya mwenyekiti katika mashirika ya umma zaidi ya mawili au mjumbe katika vyombo vya usimamizi zaidi ya vitatu; na

(c) ana sifa stahiki zilizoainishwa katika sheria husika.

(3) Bila kujali masharti mengine ya kifungu hiki, endapo nafasi inayokusudiwa kujazwa ni ya mwakilishi wa taasisi au mtu husika, Mamlaka itatekeleza wajibu wake chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa kushauriana na taasisi au mtu anayepaswa kuwakilishwa.

(4) Kwa madhumuni ya kuwezesha uteuzi au ujazaji wa nafasi zilizo wazi kwa wakati, Mamlaka itahakikisha kuwa majina yaliyopatikana ya watu wenye sifa za kuteuliwa yanawasilishwa kwa mamlaka ya uteuzi ndani ya kipindi cha miezi sita kabla ya kuisha kwa muda wa kuhudumu wa mtu anayeshika nafasi inayokusudiwa kujazwa.

Baadhi ya watu kukosa sifa

**17.-**(1) Mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kama mwenyekiti au mjumbe katika chombo cha usimamizi wa shirika la umma ikiwa mtu huyo ni-

(a) waziri;
(b) Katibu Mkuu;
(c) mbunge;
(d) Mkuu wa Mkoa;
(e) Mkuu wa Wilaya; au
(f) diwani.

(2) Mtu yeyote aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) ambaye, mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii anashika nafasi ya mwenyekiti au mjumbe katika chombo cha usimamizi, atamalizia muhula wake katika nafasi anayoshika, isipokuwa kwamba hatakuwa na sifa za kuteuliwa tena.

Rejesta ya mashirika ya umma

**18**. Mamlaka itatunza na kuhifadhi rejesta ya mashirika ya umma ambayo itajumuisha-

(a) orodha ya mashirika ya umma;
(b) majina na wasifu wa watendaji wakuu, wenyeviti na wajumbe wa vyombo vya usimamizi wa mashirika ya umma; na
(c) taarifa nyingine ambazo Mamlaka itaona ni muhimu.

Mamlaka ya kuitisha taarifa

**19**.-(1) Mamlaka inaweza kumtaka mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi au afisa wa shirika la umma kuwasilisha taarifa yoyote kwa utaratibu na ndani ya muda utakaoainishwa kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

(2) Endapo mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi au afisa wa shirika la umma, bila sababu za msingi, atashindwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) ndani ya muda ulioainishwa au atatoa taarifa za uongo au za kupotosha, Mkurugenzi Mtendaji anaweza kupendekeza-

(a) kwa mamlaka ya uteuzi kumuondoa madarakani mtendaji mkuu au mweyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi; au
(b) hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya afisa wa shirika la umma.

(3) Kabla ya kutoa mapendekezo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), Mkurugenzi Mtendaji atamtaka mtendaji mkuu, mweyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi, ndani ya muda ulioainishwa, kueleza sababu kwanini mapendekezo hayo yasitolewe.

(4) Bila kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, mtu ambaye mapendekezo yametolewa dhidi yake chini ya kifungu hiki hatapendekezwa kwa ajili ya uteuzi kwa kipindi kingine kuwa mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi wa shirika la umma.

Ukomo wa gharama za uendeshaji

**20**.-(1) Bila kuathiri sheria yoyote inayoelekeza vinginevyo, gharama za uendeshaji wa shirika la umma, tofauti na mishahara, hazitazidi asilimia sitini ya makusanyo ya fedha za shirika la umma katika mwaka husika wa fedha.

(2) Shirika la umma litawasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali bakaa iliyopatikana baada ya kutoa gharama za uendeshaji zilizoruhusiwa katika kifungu kidogo cha (1), kwa namna itakavyoainishwa katika kanuni.

## SEHEMU YA NNE
## MFUKO WA UWEKEZAJI WA UMMA

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma

**21**.-(1) Unaanzishwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Uwekezaji wa Umma.

(2) Vyanzo vya fedha za Mfuko vitajumuisha-

(a) fedha zitakazopatikana kutoka katika gawio na michango ya mashirika ya umma na biashara au uwekezaji ambao Serikali inamiliki hisa;

(b) fedha zitakazotokana na mauzo ya hisa zinazomilikiwa na Serikali;

(c) faida itakayotokana na uwekezaji utakaofanywa na Mamlaka;

(d) misaada na michango kutoka kwa watu binafsi, makampuni au mashirika ya kimataifa; na

(e) fedha zitakazowekwa katika Mfuko kutoka katika vyanzo vingine vyovyote.

(3) Waziri mwenye dhamana ya fedha, baada ya kushauriana na Waziri, na kwa kuzingatia utaratibu wa uidhinishaji wa bajeti, atabainisha kiwango cha fedha zitakazolipwa katika Mfuko chini ya kifungu kidogo cha (2)(a) na (b).

Madhumuni ya Mfuko

**22**. Malengo na madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni-

(a) kugharamia uwekezaji unaofanywa na Serikali;

(b) kuwezesha mashirika ya umma yenye ukosefu wa mitaji katika fursa za uwekezaji zenye tija; na

(c) kugharamia uendeshaji wa Mamlaka.

Usimamizi wa Mfuko

**23**.-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa msimamizi wa Mfuko.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), fedha zitatolewa katika Mfuko kwa idhini ya Kamati ya Uongozi.

Utunzaji wa kumbukumbu na ukaguzi wa Mfuko

**24**.-(1) Mkurugenzi Mtendaji atahakikisha kuwa hesabu na kumbukumbu zinazohusu Mfuko zinatunzwa kwa usahihi.

(2) Mfuko utakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kamati ya Uongozi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma

**25**.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Uongozi itakayojulikana kama Kamati ya Uongozi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma.

(2) Kamati ya Uongozi itakuwa na wajumbe tisa kama ifuatavyo:

(a) Katibu Mkuu Kiongozi, ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya fedha;
(c) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya uwekezaji;
(d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(e) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya sera, bunge na uratibu;
(f) Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; na
(g) wajumbe wengine watatu wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uwekezaji na biashara, watakaoteuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Mamlaka.

(3) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa Katibu wa Kamati.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu katika kifungu hiki na kwa kuzingatia utaratibu utakaowekwa na Kamati, wajumbe wa Kamati ya Uongozi watahudhuria vikao vyote vya Kamati wao binafsi.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, Kamati ya Uongozi itaamua na kusimamia utaratibu wa kuendesha shughuli zake.

Majukumu ya Kamati ya Uongozi

**26**. Kamati ya Uongozi, miongoni mwa masuala mengine-

(a) itaamua kiwango cha uwekezaji wa Serikali katika eneo husika;
(b) itaidhinisha mashirika ya umma yanayohitaji kuwezeshwa kifedha;
(c) itajadili na kupitisha mikakati ya kuimarisha

mashirika ya umma; na

(d) itaidhinisha mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Mamlaka

**27**. Fedha za Mamlaka zitajumuisha-

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Bunge;

(b) misaada, mikopo au michango yoyote kwa Mamlaka;

(c) fedha zitakazopatikana kutokana na huduma zitakazotolewa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii au sheria nyingine yoyote;

(d) fedha kutoka katika Mfuko; na

(e) fedha nyingine itakayolipwa kwa Mamlaka chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote.

Hesabu na ukaguzi

Sura ya 348

**28**.-(1) Mamlaka itatunza vitabu sahihi vya hesabu na kumbukumbu nyingine zinazohusiana na shughuli zake na kuandaa taarifa ya hesabu ya mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma.

(2) Hesabu za Mamlaka zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au afisa aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Taarifa ya mwaka

**29**.-(1) Ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha, Mamlaka itaandaa taarifa ya mwaka kuhusiana na mwaka wa fedha uliopita na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri ambaye ataiwasilisha Bungeni.

(2) Taarifa ya mwaka itajumuisha-

(a) maelezo ya kina kuhusu utendaji wa Mamlaka kwa mwaka husika;

(b) nakala ya hesabu za Mamlaka zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyingine yoyote ambayo Mamlaka itahitajika kutoa chini ya Sheria hii.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

Makosa na adhabu

**30**. Mtu ambaye-
(a) atakaidi wito rasmi wa Mamlaka; au
(b) atamzuia afisa wa Mamlaka kutekeleza wajibu wowote chini ya Sheria hii,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kanuni

**31**. Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufutwa kwa Sheria na masharti ya muendelezo Sheria Na. 35 ya mwaka 1959

**32**.-(1) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina inafutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1), jambo lolote lililofanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina litabaki kuwa halali hadi pale litakapobatilishwa au kubadilishwa chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, kanuni, miongozo au sheria ndogo nyingine zozote zinazohusu uwekezaji wa umma na usimamizi katika mashirika ya umma ambazo zinaendelea kutumika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii zitaendelea kutumika kana kwamba zimetengenezwa chini ya Sheria hii, kwa kiwango ambacho hazikinzani na masharti ya Sheria hii, hadi pale zitakapobadilishwa au kufutwa.

Masharti ya mpito

**33**. Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii-
(a) watumishi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina watachukuliwa kuwa ni watumishi wa Mamlaka;
(b) mali na madeni yote ya Msajili wa Hazina yatakuwa ya Mamlaka;
(c) masuala yote yaliyokuwa yanashughulikiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo hayajakamilika yataendelea kushughulikiwa na Mamlaka hadi pale yatakapokamilika.

Marekebisho ya jumla

**34**. Mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii-
(a) rejea yoyote ya Msajili wa Hazina katika sheria yoyote itachukuliwa kuwa ni rejea ya Mamlaka au Mkurugenzi Mtendaji, kadri itakavyokuwa; na

Sheria Na.

(b) rejea yoyote ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya

35 ya mwaka 1959

Msajili wa Hazina itachukuliwa kuwa ni rejea ya Sheria ya Uwekezaji wa Umma.

SEHEMU YA SABA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma, (Sura ya 257)*

Ufafanuzi Sura ya 257

**35**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 12

**36**. Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 12 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:

"Limitation of appointment as chief executive, chairperson or member of governing body

**12**.-(1) A person shall not be appointed-

(a) to be a chairperson of more than two Boards or a member of more than three Boards at the same time, unless such person is a chairperson or a member by virtue of his office; and

(b) to be a chief executive, chairperson or member of a governing body if such person is disqualified under any written law.

(2) Every proposed appointment shall, prior to submission to the appointing authority, be forwarded to the Public Investment Authority for the purpose of giving effect to the provisions of this section.".

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, (Sura ya 348)*

Ufafanuzi Sura ya 348

**37**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu"

Marekebisho ya kifungu

**38**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 6A(2)-

(a) kwa kufuta maneno "utilization and disposal"

cha 6A

yaliyopo katika aya (a) na badala yake kuweka maneno "and utilisation";

(b) kufuta aya (d); na

(c) kubadili mpangilio wa aya (e) na (f) kuwa aya (d) na (e), mtawalia.

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Kuunda Upya na Kuhamisha Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, (Sura ya 404)*

Ufafanuzi Sura ya 404

**39**. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuunda Upya na Kuhamisha Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 3

**40**. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 3-

(a) kwa kufuta tafsiri ya maneno "ATHCO", "Board", "Commission", "Committee" "Corporation", "LART", "SIMU 2000", "transitional period" na "Tribunal";

(b) kwa kufuta maneno "the Bureau or the Corporation" yaliyopo katika tafsri ya maneno "designated new entity" na badala yake kuweka maneno "or the Bureau";

(c) kwa kufuta maneno "and includes the assets of LART, ATHCO and SIMU 2000" yaliyopo katika tafsri ya maneno "residual assets"; na

(d) kwa kufuta maneno "the NMB or the Corporation, as the case may be" yaliyopo katika tafsiri ya maneno "vesting date" na badala yake kuweka maneno "or the NMB".

Kufutwa kwa Sehemu ya Pili

**41.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta Sehemu ya Pili.

Kufutwa kwa vifungu vya 12 na 13

**42.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta vifungu vya 12 na 13.

Kufutwa kwa Jedwali la Pili

**43**. Sheria Kuu inarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Pili.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9(4))*

**TARATIBU ZA BODI YA MAMLAKA**

Muda wa kuhudumu

**1.-**(1) Mjumbe wa Bodi, isipokuwa kama atajiuzulu au uteuzi wake kutenguliwa, atashika madaraka kwa kipindi cha miaka minne kutoka tarehe ya kuteuliwa na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine.

(2) Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu baada ya kutoa notisi ya siku thelathini kwa maandishi kwenda kwa Waziri.

(3) Waziri anaweza kujaza nafasi yoyote itakayokuwa wazi katika ujumbe wa Bodi, na anaweza kutengua uteuzi wa mjumbe yeyote, na kuteua mjumbe mwingine badala yake kulingana na uwakilishi uliopo.

Vikao vya Bodi

**2.-**(1) Bodi itakutana angalau mara nne kila mwaka.

(2) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (3), masuala yatakayojadiliwa katika kikao cha Bodi yataamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliopo na waliopiga kura, na pale ambapo kura zitalingana, Mwenyekiti au mtu yeyote anayeongoza kikao husika atakuwa na kura ya turufu juu ya kura yake ya uamuzi.

(3) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (2), endapo Mwenyekiti ataelekeza, uamuzi unaweza kufanywa na Bodi bila kikao kwa kusambaza nyaraka husika miongoni mwa wajumbe na maoni ya wajumbe kwa maandishi yatakuwa uamuzi wa Bodi, isipokuwa mjumbe yeyote anaweza kuomba uamuzi usubiri na suala hilo lijadiliwe katika kikao cha Bodi.

Akidi

**3**. Akidi katika kikao chochote cha Bodi itakuwa nusu ya wajumbe waliopo.

Mihtasari ya vikao

**4.-**(1) Katibu ataandika na kutunza mihtasari ya shughuli zote zinazotekelezwa katika kikao na mihtasari ya kila kikao cha Bodi itasomwa na kuthibitishwa au kusahihishwa na kuthibitishwa katika kikao cha Bodi kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti au mtu anayeongoza kikao husika, na Katibu.

(2) Muhtasari wa kikao cha Bodi uliosainiwa na Mwenyekiti au mtu aliyeongoza kikao na Katibu, isipokuwa pale ambapo kasoro itathibitishwa, utachukuliwa kama kumbukumbu

sahihi ya kikao kinachohusika na muhtasari huo.

Uhalali wa shughuli

**5**. Uhalali wa kitendo au shughuli yoyote ya Bodi hautabatilishwa kutokana na uwazi katika nafasi ya mjumbe yeyote au kwa sababu ya kasoro yoyote katika uteuzi wa mjumbe.

Stahili za wajumbe

**6**. Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi watalipwa stahili kama zitakavyoamuliwa na mamlaka husika.

Bodi inaweza kusimamia shughuli zake

**7.** Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Bodi inaweza kusimamia shughuli zake.

**MADHUMUNI NA SABABU**

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji wa Umma ya Mwaka 2023 kwa lengo la kuimarisha na kuweka masharti bora ya usimamizi wa uwekezaji katika mashirika ya umma. Sheria inayopendekezwa inakusudia kutatua changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mamlaka na majukumu ya Msajili wa Hazina, ikiwemo kukosekana kwa utaratibu madhubuti wa upatikanaji wa Wakuu wa Mashirika ya Umma na wajumbe wa Bodi za mashirika ya umma, utaratibu wa uhamishaji wa mali za mashirika kutoelezwa bayana, kukosekana kwa vyanzo vya uhakika vya fedha kwa ajili ya uwekezaji na muingiliano wa kimamlaka katika kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kwa mashirika ya umma. Hivyo, Sheria inayopendekezwa kutungwa itajumuisha masharti mbalimbali yatakayotoa ufumbuzi wa changamoto hizo ili kuwezesha mashirika ya umma kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Saba.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka masharti ya utangulizi ambayo ni Jina la Muswada, utaratibu wa kuanza kutumika kwa Sheria, mawanda ya matumizi yake na tafsiri ya misamiati iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu masharti ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma. Sehemu hii inaainisha mamlaka na majukumu ya Mamlaka inayopendekezwa kuanzishwa, uteuzi wa Bodi ya Mamlaka, Mkurugenzi Mtendaji pamoja na masharti kuhusu watendaji wengine. Kwa mujibu wa masharti ya Muswada, Mamlaka inayopendekezwa kuanzishwa itarithi majukumu ya Msajili wa Hazina na miongoni mwa majukumu hayo ya msingi ni kusimamia utendaji wa mashirika ya umma, kuishauri Serikali kuhusu uanzishaji au ufutaji wa mashirika ya umma, kuhakikisha michango na gawio kutoka mashirika ya umma na kampuni ambayo Serikali inamiliki hisa inalipwa kwa wakati, kubaini maeneo yenye tija kwa Serikali kuwekeza na kufanya mapitio na kuidhinisha maslahi ya wajumbe wa vyombo vya usimamizi wa mashirika ya umma kwa kushauriana na Wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu usimamizi wa mashirika ya umma. Miongoni mwa masharti hayo ni pamoja na utaratibu wa upatikanaji wa majina kwa ajili ya uteuzi katika nafasi za watendaji wakuu wa mashirika ya umma au wenyeviti au wajumbe wa vyombo vya usimamizi wa mashirika ya umma na utaratibu wa uhamishaji wa mali za mashirika ya umma. Ili kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanaendeshwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyowekwa, inapendekezwa kuwa uteuzi wa watendaji wakuu,

wajumbe na wenyeviti wa vyombo vya usimamizi wa mashirika ya umma ufanyike kwa kuzingatia njia ya ushindani. Aidha, kwa mujibu wa masharti yanayopendekezwa katika Sehemu hii, mtu hatakuwa na sifa za kushika nafasi ya mjumbe au mwenyekiti wa chombo cha usimamizi wa shirika la umma ikiwa mtu huyo ni waziri, Katibu Mkuu, mbunge, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya au diwani. Sehemu hii pia inaweka masharti kuhusu ukomo wa gharama za uendeshaji wa shirika la umma. Masharti hayo yanaeleza kuwa gharama za uendeshaji wa shirika hazipaswi kuzidi asilimia sitini ya makusanyo ya fedha za shirika la umma katika mwaka husika wa fedha.

Sehemu ya Nne ya Muswada inaweka masharti ya uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ambao unakusudiwa kuwa chanzo cha uhakika cha kugharamia uwekezaji mbalimbali unaofanywa na Serikali, kukwamua na kuwezesha mashirika ya umma yenye ukosefu wa mitaji katika fursa za uwekezaji wenye tija na kugharamia uendeshaji wa Mamlaka. Sehemu hii pia inaweka masharti ya vyanzo vya fedha za Mfuko ambavyo ni gawio na michango ya mashirika ya umma, mauzo ya hisa, faida itakayotokana na uwekezaji, misaada na fedha zitakazowekwa katika Mfuko huo kutoka katika vyanzo vingine vyovyote. Aidha, inapendekezwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ndiye awe msimamizi wa Mfuko na katika majukumu yake atawajibika kwa Kamati ya Uongozi wa Mfuko. Sehemu hii pia inaanzisha Kamati ya Uongozi wa Mfuko pamoja na kuainisha wajumbe na madhumuni yake.

Sehemu ya Tano ya Muswada inaweka masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya fedha za Mamlaka na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu za Mamlaka. Vyanzo vya fedha vinavyopendekezwa vinajumuisha fedha zitakazoidhinishwa na Bunge na fedha zitakazotokana na huduma zitakazotolewa na Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake. Kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Serikali, Sheria pendekezwa inaweka takwa kuwa hesabu za Mamlaka zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Sehemu ya Sita ya Muswada inaainisha masharti mengineyo ambayo ni pamoja na makosa na adhabu kwa watakaokiuka masharti ya Sheria inayopendekezwa na mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni. Sehemu hii pia inapendekeza kufuta Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ya Mwaka 1959 na kuweka masharti ya mpito baada ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa. Aidha, inapendekezwa pia katika Sehemu hii kuwa rejea yoyote ya Msajili wa Hazina katika Sheria yoyote itachukuliwa kuwa ni rejea ya Mamlaka au Mkurugenzi Mtendaji, kulingana na mazingira husika na rejea yoyote ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina itachukuliwa kuwa ni rejea ya Sheria hii inayopendekezwa kutungwa.

Sehemu ya Saba ya Muswada inahusisha marekebisho ya Sheria mbalimbali ambazo ni Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Sheria ya Mashirika ya Umma,

Sura ya 257 na Sheria ya Kuunda Upya na Kuhamisha Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, Sura ya 404. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha masharti ya Sheria hizi na Sheria inayopendekezwa kutungwa ili kuhakikisha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria na kuleta ufanisi wa mfumo wa kisheria na kitaasisi unaopendekezwa.

Dodoma,
17 Oktoba, 2023

**KITILA A. MKUMBO**
*Waziri ya Nchi-Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*